**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

**TUME YA UTUMISHI SERIKALINI**

**Kumb.Na.BA.1/25/02/81** **14 Novemba, 2024**

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Tume ya Utumishi Serikalini inatangaza nafasi za kazi za **Afisa Vipimo Daraja la II ZPSI - 06 (Nafasi 3 – Unguja na Nafasi 1 Pemba)** kwa ajili ya **Wakala wa Vipimo Zanzibar**:-

## ***Sifa za Muombaji:***

1. Awe Mzanzibari mwenye umri usiozidi miaka arobaini na sita 46.
2. Awe na Vyeti halisi vya kumalizia Masomo.
3. Awe amehitimu shahada ya kwanza katika fani ya metrolojia kutoka katika chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

## ***Majukumu:***

1. Kutunza vifaa vya kitaalamu katika karakana za vipimo.
2. Kukagua vipimo au mizani.
3. Kuangalia na kudhibiti vipimo.
4. Kurekebisha mawe ya mizani ambayo yamepungua au kuzidi uzito.
5. Kupokea maoni na hoja za wananchi, kuzifuatilia na kutoa taarifa kwa mamlaka husika kwa lengo la kufanyiwa kazi.
6. Kuandika ripoti za utekelezaji wa kazi ikiwemo ripoti ya robo, nusu na mwaka.
7. Kufanya kazi nyengine zinazolingana na majukumu yake kama atakavyopangiwa na Mkuu wake.

## ***Jinsi ya Kuomba:***

- Maombi yote yawasilishwe kwa njia ya Kielektroniki kwenye mfumo wa Maombi ya Ajira (ZanAjira) kupitia anuani ifuatayo: **https://portal.zanajira.go.tz** kuanzia tarehe **14 Novemba, 2024** hadi tarehe **28 Novemba, 2024**.
- Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti ya Tume ya Utumishi Serikalini **www.zanajira.go.tz**.
- Barua za maombi zitumwe kwa anuani ifuatayo kupitia mfumo wa ZanAjira (kwa njia ya kielektroniki pekee):-

  **KATIBU,**<br>
  **TUME YA UTUMISHI SERIKALINI,**<br>
  **S.L.P 1587,**<br>
  **ZANZIBAR**
- Muombaji anatakiwa kuainisha nafasi ya kazi anayoiomba.
- Muombaji atakaewasilisha “Progressive Report” au “Statement of Results” pekee maombi yake hayatazingatiwa.
- Kwa msaada wa kitaalamu wasiliana na Tume ya Utumishi Serikalini kupitia simu Nam. 0773101012.

**TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA:**<br>
**KATIBU,**<br>
**TUME YA UTUMISHI SERIKALINI.**